NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

Ridván 2017

Kwa Wabaha'i wa Ulimwengu

Marafiki Wapendwa sana,

Ona jinsi jumuiya ya Jina Kuu Kabisa iinukavyo! Kwa mwaka mmoja tu uliomalizika tangu uanzishwaji wa Mpango mpya, taarifa hushuhudia juu ya kiwango cha kile kinachojaribiwa na kinachoanza kukamilika. Ili kuleta nguvu kubwa zaidi kwa programu 5,000 za ukuaji kunadai kiwango cha jitihada isiyokuwa na historia kabisa. Pamoja na ushikiliaji thabiti wa kanuni za kimsingi za Mpango, idadi kubwa ya marafiki wanatekeleza mahitaji yake, wakionesha msimamo na dhabihu katika ubora wa muitiki wao. Kama ilivyotazamiwa, baadhi ya programu za ukuaji wenye nguvu ambazo zimekuwa zikidumishwa kwa muda mrefu, zinakuwa mabwawa ya maarifa na rasilimali, zikitoa msaada kwa maeneo yazizungukazo na kurahisisha usambazaji wa haraka wa tajiriba (uzoefu) na umaizi. Vituo vya shughuli zenye nguvu—ule ujirani na vijiji ambako kazi ya ujenzi wa jumuiya imetiliwa nguvu nyingi sana—inathibitisha kuwa eneo oevu kwa ajili ya mbadiliko wa pamoja. Kikosi kilichopanuliwa zaidi na chenye nguvu cha Washauri Wasaidizi na wasaidizi wao kinachochea jitihada za waumini, kikiwasaidia kupata muono wa jinsi ya kuendeleza mchakato wa ukuaji katika mazingira mbalimbali na kuainisha mbinu ambazo hukidhi hali ndani ya kila klasta. Zikisaidiwa na Mabaraza yao husika ya Kiroho ya Kitaifa, Halmashauri za Kibaha'i za Kanda zinajifunza jinsi gani kasi ya Mpango inavyoweza kujengwa kupitia msafa katika klasta mbalimbali kwa mmoja, ambapo katika baadhi ya nchi ndogo zaidi zisizo na Halmashauri, vyombo vipya kwenye ngazi ya kitaifa vinaanza kufanya vivyo hovyo. Ingawa, kama ambavyo ingeweza kutarajiwa kwa mchakato wowote hai na unaokua, maendeleo ya kasi yanayoshuhudiwa katika baadhi ya sehemu hayatatokea kwingineko, jumla ya idadi ya programu za ukuaji wenye nguvu ulimwenguni tayari inaanza kupanda. Zaidi, tunafurahi kuona kwamba ushiriki katika shughuli za Mpango umeongezeka kwa udhahiri katika duru zake nne za mwanzo.

Ishara zisingeweza kuwa za kutarajiwa zaidi, wakati huo, kwa kile ambacho kingeweza kuletwa na mwaka ujao. Na je, ni nini kinachoweza kustahili zaidi kumtolea Uzuri Uliobarikiwa kwenye kumbukumbu ya miaka mia mbili ya kuzaliwa Kwake kuliko jitihada ya dhati ya wapendwa Wake ya kuongeza ufikiwaji wa Imani Yake? Ya kwanza kati ya sherehe mbili pacha inayotarajiwa kusherehekewa na ulimwengu wa Kibahá'í hivyo ni tukio lenye matarajio ya kusisimua mno. Ukitazamwa bara bara, mwaka huu hutoa fursa moja kubwa kabisa ya ulimwengu mzima ambayo haijawahi kutokea, kwa ajili ya kuiunganisha mioyo kwa Bahá'u'lláh. Katika miezi ijayo, hebu sote tuwe wafahamivu wa nafasi hii ya thamani na tuwe macho kwa fursa zinazoweza kujitokeza katika kila nafasi kwa ajili ya kuwafahamisha wengine juu ya maisha na utume Wake adhimu. Kwa fursa ya ufundishaji ambayo hivi sasa ipo mbele ya ulimwengu wa Kibaha'i kuweza kutwaliwa kwenye kiwango chake kikamilifu, mawazo ya kiubunifu huhitaji kutolewa kwenye maongezi ambayo yangekunjuka na kila aina ya mtu. Wakati wa maongezi ya maana kama hayo, uelewa huinuliwa na mioyo hufunguliwa—wakati mwingine papo hapo. Katika kazi hii yenye thamani wote hupata wito, na kwa shangwe ambayo hutokana na kujihusisha katika kazi hii

ambayo pasiwepo wa kujinyima mwenyewe. Tunamsihi Yule Mpendwa mmoja kwamba mwaka wote huu wa kutimiza sherhe ya miaka mia mbili uweze kujazwa na shangwe ambayo ni safi na tamu kabisa: ya kuiambia roho nyingine juu ya mapambazuko ya Siku ya Mungu.

Wajibu ambao lazima utimizwe na kundi la waaminifu unashinikizwa zaidi na hali ya machafuko, kutoaminiana, na wingu lililotanda ulimwenguni. Kwa kweli, marafiki wanapaswa kutumia kila fursa kuangazia nuru ambayo inaweza kumulika njia na kuwapa uhakika wale wenye mashaka, tumaini kwa wanaokata tamaa. Tunakumbushwa juu ya ushauri uliotolewa na Mlezi kwa jumuiya moja ya Kibaha'i kwa maneno ambayo huonekana yalikusudiwa kwa ajili ya wakati wetu: "Wakati mfumo wa jamii ya siku hizi unavyong'oka na kuvunjika chini ya mkazo na msongo wa matukio ya kutisha na majanga, kadiri nyufa zitiavyo mkazo mpasuko unaotenganisha taifa kutoka taifa, tabaka kutoka tabaka, mbari kutoka mbari, na itikadi kutoka itikadi, zinavyoongezeka, watendaji wa Mpango sharti wadhihirishe mshikamano mkubwa zaidi katika maisha yao ya kiroho na shughuli za kiutawala, na kuonesha kiwango cha juu zaidi cha jitihada za pamoja, cha kusaidiana, na cha maendeleo patanifu katika shughuli zao za pamoja." Daima wakisisitizia juu ya umuhimu wa kiroho wa kazi ya Imani na dhamira yenye lengo moja ambayo kwayo waumini wanapaswa kutekeleza majukumu yao matakatifu, Shoghi Effendi vile vile alionya dhidi ya kuwa na sehemu yoyote katika mabishano ya kisiasa, mitego na magomvi. "Acha wainuke juu ya umaalum wote na ufuasi wa vyama.," yeye aliasa mahali pengine, "juu ya mabishano yasiyo ya maana, hila ndogo ndogo, tamaa za mpito vinavyoufadhaisha uso, na kuushughulisha ulimwengu unaoendelea kubadilika." Haya ni mapovu na manyunyu yasiyoepukika yanayorushwa kama wimbi baada ya wimbi likiitetemesha jamii yenye zahama na iliyogawanyika. Ni mengi mno ya kuweza kuhangaikiwa pamoja na masumbufu ya aina hii. Kama kila mfuasi wa Bahá'u'lláh ajuavyo fika, hatma ya ustawi wa binadamu inategemea juu ya tofauti zake kuweza kuvukwa na umoja wake kusimamishwa imara. Kila mchango anaoutoa Mbaha'i kwa maisha ya maisha ya jamii yao umekusudiwa kukuza umoja; kila jitihada ya ujenzi wa jumuiya inaelekezwa kwenye kusudi hilo hilo. Kwa wale waliochoshwa na ugomvi, jumuiya zinazokua chini ya kivuli cha Jina Kuu Kabisa hutoa mfano wenye nguvu wa kile ambacho umoja unaweza kutimiza.

Tunatoa sifa kwa Bwana wa Mabwana kwa kuona wengi wa wapendwa Wake, katika namna nyingi, wakijitoa vyote ili bendera ya umoja wa binadamu iweze kuinuliwa juu. Marafiki mpendwa mno: Wakati mwaka wenye heri kabisa uanzavyo sasa, je, isingewezekana kila mmoja wetu kutafakari ni nini matendo ya mbinguni ambayo rehema Zake zaweza kutusaidia kutenda?

*Umesainiwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*